**336/1**
**Lugha ya**
**Kiswahili**
**Julai 2024**
**Paper 1**

**2 Hours**

**BUGANDA EXAMINATION COUNCIL MOCKS 2024**

# Uganda Certificate of Education

LUGHA YA KISWAHILI 336/1

**INSHA NA UFUPISHO**

MUDA: SAA MBILI

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA:**

- *Karatasi hii ina sehemu;* **mbili**: **A** *na* **B**.
- *Jibu maswali* **mawili** *kwa ujumla.*
- *Sehemu* **A**, *kuna maswali mawili. Chagua swali* **moja**.
- *Sehemu* **B** *ni ya* **lazima kwa watahiniwa wo**

**Pindua**



© *Buganda Examination Council Mocks 2024*

## SEHEMU A:

UTUNZI WA INSHA

**AMA**

1. Wakulima wengi nchini Uganda huathiriwa na mabadiliko ya hali ya anga. Hali hii huwasababishia hasara kubwa na kupelekea bei ya mazao kupanda na kushuka sokoni. Wewe kama afisa wa utabiri wa hali ya anga, wape ushauri wakulima kuhusu jinsi ya kukabiliana na hali hii.

**AU**

2. Mwalimu mkuu wa shule yako ametangaza mkutano wa dharura wa wazazi wa wanafunzi wa kidato cha nne. Mkutano huu ni muhimu sana na hivyo, watahiniwa wote wameambiwa kuwaarifu wazazi wao mapema iwezekanavyo.
   **Wewe kama mtahiniwa, mpashe habari mzazi wako kuhusu mkutano huu.**

## SEHEMU B:    UFUPISHO

3. **Fupisha taarifa hii kwa maneno 100 ukizingatia 'Umuhimu wa viumbe'**

Dunia hii ina viumbe wa aina nyingi. Viumbe wana umuhimu usiohesabika kwa mwanadamu. Hebu tutazame kwa undani viumbe hawa watatu;- wanyama, ndege na wadudu. Kuna wanyama wa aina mbili; wanyama-pori na wanyama wanaofugwa nyumbani. Wanyama-pori wanakaa kwenye mbuga za wanyama misituni/porini/mwituni na majini. Ikumbukwe pia kuna hifadhi za wanyamapori ambapo wanyamapori hufugwa na binadamu. Wanyama wanaokaa misituni au porini ni kama vile; Simba, chui, Tumbili, Kifaru, swala, Nyati, Tembo, kuchakuro, Twiga, Pundamilia, Fisi, Mbweha, nakadhalika. Kwa nchi kama Uganda wanyamapori wanasaidia nchi kuingiza pesa za kigeni kutoka kwa watalii wanaokuja kuwatazama. Watalii hao hulipa pesa nyingi kwa shughuli hiyo. Pia kuna wanyama pori wanaokaa majini kama; Samaki, Mamba na Kiboko.

Kuna wanyama wanaofugwa nyumbani kwa binadamu. Miongoni mwa wanyama wanaofugwa ni; Ng'ombe, Mbuzi, Mbwa, kondoo, punda, Ngamia, Nguruwe, Sungura , paka, panya na farasi. Wanyama hawa ni muhimu sana. Wanyama wanaleta faida kubwa


*© Buganda Examination Council Mocks 2024*

mno kwa binadamu. Kwa mfano; Wanyama wanatupatia nyama ambayo ni chakula kwa binadamu, Wakulima wanapata pesa nyingi baada ya kuuza wanyama sokoni, wanyama wanafanya kazi kubwa ya kusafirisha watu na kubeba mizigo mizito, wanyama wanatupatia siagi na maziwa ya kunywa, Ngozi za wanyama zinasaidia binadamu kutengeneza viatu, ngoma, mikoba, nguo, kofia na silaha. Wanyama wanafanya kazi ya kulinda mali kama askari polisi nyumbani kwa binadamu.

Ndege au nyuni ni wa aina mbili; kuna ndege pori na ndege wanaofugwa nyumbani. Ndege wanaokaa porini au mwituni ni kama; Mbuni, kanga, korongo, Tausi, Kwale, tai, kipanga, Bundi, Mwewe na kadhalika. Ndege wanaofugwa nyumbani ni kama vile; Kuku, Bata, Kasuku, Batamzinga na Njiwa. Umuhimu wa ndege kwa binadamu ni kama; Kupata nyama ambayo ni chakula kwa binadamu, Ndege wanapatia binadamu mayai ya kula, Binadamu anapata pesa nyingi baada ya kuuza ndege, mayai na nyama ya ndege.

Kundi lingine la viumbe ni wadudu. Kuna wadudu wengi sana duniani kwa mfano; Mchwa, kumbikumbi, senene, panzi, kipepeo, kiwavi, siafu, sisimizi, kupe, funza, nyuki, Nzi, Mbu, Mende, mabuu, nakadhalika. Wadudu wana faida na *madhara chungu nzima*. Kwa upande wa faida za wadudu hao; Nyuki wanatengeneza asali ambayo ni tamu sana. Mara binadamu husema, “tamu kama asali”. Hii inamaanisha kwamba asali ni muhimu sana kwake mwanadamu mpaka akaiundia tashibihi kutokana na utamu wake. Wadudu pia ni chakula muhimu kwa binadamu na viumbe wengine.

Mungu aliumba viumbe duniani kwa imani ya ‘Lisha ulshwe’ haswa! Viumbe hulana na kufaana katika kujengeana maisha. Wanadamu wengi wanakula wadudu kama vile; Kumbikumbi, mchwa na Senene. Kwa upande wa uhatari au mambo mabaya ya wadudu (madhara); wadudu wanasambaza ugonjwa kwa binadamu. Kwa mfano; Mbu wanasambaza ugonjwa wa malaria. Nzi wanasambaza ugonjwa wa kipindupindu na waba. Wadudu wengine wanasumbua sana mwanadamu wanang’ata, wanauma, wanawasha na kuleta madhara na maumivu makubwa kwa mwili wa binadamu.

***MWISHO***


© *Buganda Examination Council Mocks 2024*